IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI



**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 21 May 2002 (afternoon)
Mardi 21 mai 2002 (après-midi)
Martes 21 de mayo de 2002 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.

*Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:*

**1.** (a)

| | |
|---|---|
| Fedha unapodaiwa | hata iwe milioni |
| Utafanya kila njia | uzilipe kwa yakini |
| Hisani ukifanyiwa | utalipa kitu gani? |
| Hisani asoijua | kiumbe umuambae |
| | |
| Hisani hailipiki | hata ukafanya nini |
| Wala haikadiriki | kupimwa yake thamani |
| Hisani kama riziki | anojalia Manani |
| Hisani asoijua | kiumbe umuambae |
| | |
| Hisani siyo kupewa | kitu cha kubwa thamani |
| Hisani ni kutendewa | wema na nyingi imani |
| Hisani ukifanyiwa | u mdeni maishani |
| Hisani asoijua | kiumbe umuambae |
| | |
| Hisani asoijua | ni kiumbe hayawani |
| Jema kwake huwa baya | haijui shukurani |
| Hakuna anachopewa | yeye akakithamini |
| Hisani asoijua | kiumbe umuambae |
| | |
| Si mtu katu si mtu | asoijua hisani |
| Yuko sawa na viatu | vivaliwavyo migu'ni |
| Usitupe wako utu | kwa as'o shukurani |
| Hisani asoijua | kiumbe umuambae |

Kutoka *Jua*, na Amina Bakari, 2000

– Shairi hili linatwambia nini kuhusu mtazamo wa maisha wa mshairi?

– Katika shairi hili thamani ya vitu inalinganishika vipi na hisani?

– Mbinu gani zinazolifanikisha au kuliharibu shairi hili? Toa sababu.

**1.** (b)

Mama wa pili kutiwa mbaroni siku hiyo alikuwa na mfuko mkubwa wa plastiki uliojaa samaki waliokaushwa. Wa tatu alikuwa na ndoo iliyojaa chapati. Mama wa nne aliposhikwa alikuwa na sufuria kubwa la mahindi mabichi yaliyochemshwa. Mkuu wa kikosi cha askari wa manispaa, Koplo Marete, alitangaza kuwa kazi ya siku hiyo ilikuwa imekwisha. Basi askari wote watano walikusanyika, tayari kuwapeleka wahalifu kwa polisi. Koplo Marete alimwarifu dereva kuwa mambo yote yalikuwa tayari. Dereva aliwasha gari moto lakini hakuliendesha. Alifahamu jinsi mambo yalivyofanywa. Hapo ndipo akina mama walipoanza kujitetea na kuomba msamaha. Katika majibizano yaliyofuatia, usanifu wa Kiswahili ulikuwa na nafasi ndogo tu.

"Hee! Mnafikiri serikali ni paka mzee? Ndiyo sababu mnaifanyia mchezo huu wa paka na panya? Leo mtakiona," Koplo Marete alianza kutoa vitisho. Askari wake walimwunga mkono.

"Vichwa ngumu kama mawe. Hamsikiangi maneno ya serikali. Asiyesikia la mkuu hulalanga ndani ya seli mwishowe," mmoja alisema.

"Kwanza huyu wa mahindi! Akiagizwa kufungua mzigo wake hataki," mwingine alisema.

"Nilifungua. Mbona nyinyi askari mnapenda kutuonea," mama alijitetea. "Sasa mkitupeleka ndani watoto wetu watakula nini?"

"Sisi ni wamama masikini. Tunamwomba mutusamehe leo tu. Hata Mungu alisema tusameheane madhambi," alisihi mama mwingine.

Sasa Koplo Marete alishika usukani wa mazungumzo. "Sikilizeni akina mama," alianza. "Hatia yenu mnaijua. Adhabu mtakayoipata tukiwapeleka mbele mnaijua pia. Serikali sio mchezo. Tusipoteze wakati katika majadiliano marefu. Leo tutakubali ombi lenu la kusamehewa. Lakini mkitaka kusaidiwa nanyi muwe tayari kusaidia. Tusaidianeni. Sisi tuna njaa, nanyi mmeikosea serikali. Basi fanyeni kitu kuhusu njaa yetu."

Akina mama walianza kutafuta vibeti. Mmoja alitoa noti ya shilingi ishirini akanyoosha mkono kumpatia kiongozi wa askari. Koplo Marete alicheka kwa kejeli. "Sitaki ujinga. Mnafikiri mimi ni mtoto mdogo? Shilingi ishirini ni za kununulia peremende au nini? Kila mmoja atoe shilingi mia moja au nimwambie dereva twende mkawekwe rumande," alisema kwa ukali.

"Mia tutazitoa wapi?" Kilio cha akina mama kadha kilipaa hewani.

"Chukua hamsini," alisihi yule mama aliyeshikwa kwanza na kapu la viazi.

"Nimesema mia na sitaki mjadala, kama hamtoi mseme haraka," Koplo Marete alikuja juu.

Hatimaye akina mama walitoa hongo iliyotakwa, huku wakilalamika vikali. Waliachiliwa, wakashuka kutoka kwenye lori na kuelekea sokoni. Walikwenda kuuza vyakula vyao ambavyo sasa vilikuwa vimeondolewa viini vya kipindupindu na dawa mjarabu ya hongo. Wateja wao walilalamikia bei mpya za vyakula zilizokuja ghafula.

"Mnalalamika nyongeza ya senti hamsini tu kwa mahindi?" Aliteta yule mama aliyekuja kuuza mahindi mabichi yaliyochemshwa. "Hamjui ugumu wa kuingiza vyakula sokoni siku hizi. Leo askari wa manispaa, majambazi wakubwa – wametutoza shilingi mia kila mmoja. Sasa biashara yetu hii itakwendaje?

Kutoka *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* na Mwenda Mbatiah (mhariri), 2000

– Vipi msimamo wa mwandishi unavyojidhihirisha kuhusiana na mada inayosimuliwa katika dondoo hili?

– Dondoo hili linahusinaje na maisha yalivyo katika miji ya Afrika Mashariki?

– Zungumzia mbinu ya usimulizi kama kipengele muhimu cha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa dondoo hili.